



## BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

### ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

#### BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

#### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 31 Mei, 2023**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi  
na Dua zitasomwa.

#### I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

##### Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2023/2024.

##### Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2023/2024.

#### II. MASWALI:

##### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

72. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa azma yake nzuri ya kutujengea bandari ya Mkokotoni itakayopunguza msongamano uliopo hivi sasa katika bandari ya Malindi Unguja.

- (a) Je, kuna sababu zipi zinazopelekea kutoanza kwa safari za meli katika bandari ya Mkokotoni.
- (b) Je, tutorajie lini itaanza huduma hiyo katika Bandari ya Mkokotoni.

### **Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

233. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Wimbi la udhalilishaji wa wanawake na makundi mengine maalum maskulini, vyuoni na madrasa linazidi kuongezeka, pamoja na juhudzi za Serikali kupambana dhidi ya vitendo hivyo.

- (a) Je, ni sheria ipi makhsusi inayoshughulikia udhalilishaji wa wanawake na makundi mengine maalum maskulini, vyuoni na madrasa.
- (b) Je, ni kesi ngapi kwa kipindi cha 2020-2023 zimeripotiwa na kushughulikiwa za udhalilishaji wa wanawake na makundi mengine maalum maskulini, vyuoni na madrasa.
- (c) Je, Serikali haioni ulazima wa kutunga sheria makhsusi inayotekelzeza kwa ajili ya kushughulikia na kuondosha udhalilishaji wa wanawake na makundi mengine maalum maskulini, vyuoni na madrasa.

### **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

86. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaishukuru Serikali kwa kuajiri wananchi wake wengi. Waajiriwa wengi wasiopungua asilimia 40 wa Serikali wana kiwango cha elimu ya Stashahada (Diploma) na wanafanya kazi vizuri kwa uweledi wa hali ya juu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ufadhili wa masomo na mikopo kwa wanafunzi wenye elimu ya Stashahada ili kuijendezeza na elimu ya juu katika vyuo mbali mbali duniani.

### **Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

220. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Maadini:

Viongozi wa jimbo la Kikwajuni kwa mashirikiano na Mbunge na Mwakilishi pamoja na Madiwani, na katika kuiunga mkono Serikali kupunguza changamoto ya kupatikana maji katika jimbo la Kikwajuni, wamejenga tangi kubwa la maji katika eneo la Kikwajuni kwa Mselle. Baada ya ujenzi kukamilika tangi hilo wamekabidhiwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) zaidi ya

miaka miwili sasa lakini mpaka leo tangi hilo halijaanza kazi ya kutoa maji kwa wananchi wa Kikwajuni.

- (a) Je, ni sababu gani zimepelekea mpaka leo tangi hilo kutojazwa maji ili liweze kuwasaidia wananchi.
- (b) Lini ZAWA wanategemea kulijaza maji tangi hilo na kutoa huduma kama ilivyokusudiwa.
- (c) Wizara inatoa kauli gani ya matumaini kwa wananchi wa jimbo la Kikwajuni kuhusu kuanza huduma ya maji kwa tangi lao hilo.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,  
31 Mei, 2023.



(Raya Issa Msellem)  
KATIBU WA BARAZA